

# »Vidokezo 5 vya kukuza biringanya»

Biringanya ni mojawapo ya mboga zenye tija zaidi unazoweza kukuza kwenye bustani yako ya nyumbani kwa kuwa zinahitaji ardhi ndogo na mtaji mdogo.

Hata hivyo, inashauriwa kupanda mbegu za biringanya kwenye viriba ili zipate ukinzani mkubwa kabla ya kupandikizwa kwenye bustani kuu ili kupata mavuno zaidi. Kuna wadudu kadhaa wanaoshambulia biringanya ambao ni pamoja na vidukari na viwavi.

## Hatua za ukuzaji

Anza mchakato kwa kupanda mbegu kwenye viriba wiki 6 kabla ya mvua. Baada ya mbegu kuota, yaani siku 8–10 pandikiza miche kwenye bustani kuu.

Kisha weka mbolea ya samaki iliyochanganywa vizuri ambayo hufyonza bakteria zinazosababisha magonjwa kwenye udongo na hivyo kuhimiza uingizaji wa virutubisho kwenye mmea. Pia ongeza mbolea minyoo ya maji ambayo hujenga uwezo wa mimea kustahimili magonjwa na wadudu. Ongeza mbolea ya chumvi ya Epsom ambayo huoneza ukubwa wa biringanya, au ongeza mbolea ambazo zinaweza kufanya kazi tofauti.

Dhibiti vidukari kwa kutumia mwarobaini ambao hunyunyuziwa pande zote za majani, au tumia mchanganyiko wa sabuni na maji.

Unapopanda biringanya, chagua eneo lenye mwanga wa jua kwani mbiringanya huhitaji saa 6–8 za mwanga wa jua kwa ukuaji sahihi.

Chavusha maua kwa mkono ili kuhakikisha kwamba kila ua linakua na kuwa tunda. Pia panda aina tofauti za biringanya ili kusaidia bustani kuonekana bora na kuboresha afya ya mkulima.

Hatimaye, unapopika biringanya ongeza mbegu za binzari ya manjano ili kuongeza virutubisho.